**HOTUBA YA NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA WILLIAM TATE OLE NASHA (MB), NAIBU WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI: WAKATI WA UFUNGUZI WA MKUTANO WA SABA WA BARAZA LA WADAU WA TASNIA YA NYAMA NCHINI, TAREHE 08/03/2017, KATIKA UKUMBI WA CHUO CHA MIPANGO-DODOMA.**

---

**Mhe. Jordan Rugimbana, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,**
**Dkt. Mary S. H. Mashingo, Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi,**
**Ndugu, Doreen E. Maro, Mwenyekiti wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama,**
**Prof. Faustin P. Lekule, Mwenyekiti wa Bodi ya Nyama Tanzania,**
**Ndugu, Wajumbe wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama,**
**Ndugu, Wajumbe wa Bodi ya Nyama Tanzania,**
**Ndugu, Wawakilishi wa Wizara na Taasisi za Serikali,**
**Ndugu, Wawakilishi wa Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO),**
**Wageni Waalikwa,**
**Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo. Pia, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru waandaaji kwa kunipa fursa ya kufungua mkutano huu wa Baraza la Wadau katika Sekta Ndogo ya Nyama hapa nchini.

Napenda kuwapongeza wajumbe wote wa Baraza hili kwa kuteuliwa kuwa wawakilishi katika Baraza hili muhimu kwa maendeleo ya Nyama nchini. Naamini Mikoa, Wilaya na Taasisi mbali mbali zilizowateua zina imani kubwa nanyi ya kuiendeleza sekta ya Mifugo na hususan zao la nyama.
Aidha napenda nichukue fursa hii kuwakaribisha wote kwenye mkutano huu wa saba wa Baraza unaofanyika katika Manispaa ya Dodoma mjisikie huru kwa kipindi chote mtakachokuwa hapa. Mahudhurio yenu yanadhihirisha kukubali kwenu na kuelewa kuwa jukumu la kuendeleza sekta hii hapa nchini ni la wadau wote na ushiriki wenu ni muhimu katika kufikia lengo hilo. Mwisho napenda kushukuru viongozi wa mkoa wa Dodoma kwa kukubali kuwa wenyeji na kwa mapokezi mazuri.

**Ndugu Mwenyekiti**, nimeambiwa kwamba Baraza hili lina wajumbe wanaowakilisha wadau mbalimbali kutoka wilaya zote za Tanzania Bara, vyama vya kitaifa vya wadau, yaani wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi mbali mbali. Nina imani kwamba ninyi mlioteuliwa mtawakilisha mawazo na michango ya wadau wengine wote.

Licha ya kwamba mtakuwepo hapa kwa siku mbili tu kujadili namna ambavyo Baraza hili litasimamia utekelezaji wa Sheria ya Nyama ya mwaka 2006, naamini mtazitumia siku hizi vizuri kadri ya uwezo wenu. Kwa kuwa Baraza hili limeundwa kisheria hivyo basi, wajumbe wana jukumu kubwa la kuindeleza sekta hii kibiashara na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha zao la nyama kwa ubora na wingi katika Bara letu la Afrika na Ulimwenguni. Ni matarajio yangu kwamba endapo Baraza hili litatekeleza wajibu wake ipasavyo, tutaweza kutoa hamasa kwa wafugaji wetu kuzalisha kwa kuzingatia misingi ya kibiashara na hatimaye kuwakwamua wafugaji toka kwenye lindi la umaskini na kuongeza mchango wa sekta yetu katika pato la Taifa.

**Ndugu Mwenyekiti,** napenda sasa tuangalie uwezo wa Tanzania katika kuzalisha mifugo na biashara ya nyama. Taarifa zinaonesha kuwa Tanzania ina ukubwa wa hekta milioni **88.6** za ardhi. Aidha, katika miaka ya 1961 taarifa hizo zilieleza kuwa kati ya eneo hilo, hekta milioni **60** zinafaa kwa malisho ya mifugo. Hivi sasa eneo linalofaa kwa ajili ya malisho linakadiriwa kuwa Hekta milioni **26** tu. Kupungua kwa eneo hilo ni kutokana na ongezeko kubwa la mahitaji ya ardhi ikiwemo kukua kwa miji na ongezeko la makazi ya binadamu, mapori tengefu **28**, mbuga za wanyama kutoka mbuga mbili **(2)** hadi **16,** maeneo ya machimbo na maeneo oevu. Hivyo, eneo lililobaki halikidhi mahitaji ya sasa ya kulisha mifugo iliyopo. Hivi sasa Tanzania, inakadiriwa kuwa Ng'ombe milioni **25.8,** Mbuzi milioni **17.1,** Kondoo milioni **9.2,** Nguruwe milioni **2.67**, Kuku wa asili milioni **42.0** na wa kisasa milioni **34.5.** Aidha, mifugo hiyo kwa sehemu kubwa ni ya asili, ambayo kwa sasa inaongezeka kwa kiasi cha asilimia **3.8** kwa mwaka.
Pamoja na kupungua kwa eneo la malisho, vile vile mabadiliko ya tabianchi yanachangia kwa kasi upungufu mkubwa wa malisho. Hivyo, ili kuongeza mchango wa tasnia ya nyama katika pato la wafugaji na taifa kwa ujumla tunalazimika kubadili mfumo wa ufugaji ikiwa ni pamoja na kufuga mifugo yenye tija na kutenga, kulinda na kuendeleza nyanda za malisho. Hivi sasa

sekta ya mifugo inachangia kiasi cha asilimia **4.4** katika pato la Taifa. Pamoja na hayo, ulaji wa nyama nchini ni kilo **15** mtu kwa mwaka, hii inaonyesha kwamba watanzania wanakula kiasi kidogo cha nyama ikilinganishwa na kiwango cha kilo **50** za nyama kwa mtu kwa mwaka kilichopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO).

**Ndugu Mwenyekiti,** kutokana na takwimu hizo, ni dhahiri kwamba Tanzania ina fursa kubwa ya kuendeleza zao la nyama kibiashara na kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Takwimu za biashara ya mifugo na nyama katika mwaka 2015/2016 zinaonyesha kwamba takribani ng'ombe **1.5** milioni, mbuzi **1.2** milioni na kondoo **0.3** milioni waliuzwa. Vile vile, wastani wa **tani 648,810** za nyama (tani **323,775** nyama ya ng'ombe, tani **129,292** nyama ya mbuzi na kondoo, tani **91,451** ya nguruwe na tani **104,292** nyama ya kuku) zilizalishwa ambapo asilimia **99** ya nyama hii iliuzwa katika soko la ndani.

Aidha, soko la nyama la ndani na nje ya nchi limeendelea kukua, kwa mujibu wa takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba uwezo wa kuuza nyama na bidhaa zake nje ya nchi umeongezeka kutoka tani **25** kwa wiki (2014/2015) hadi tani **50** kwa wiki (2015/2016). Pamoja na ongezeko hilo, bado nchi yetu haijaweza kukidhi mahitaji ya nyama katika masoko ya nje (Misri tani 500 kwa wiki) na nchi za Falme za Kiarabu (UAE, tani 150 kwa wiki). Hata hivyo, taarifa zinaonesha kuwa katika mwaka 2015/2016, jumla ya tani **2,356.62** za nyama (tani **203.73** za nyama ya ng'ombe, tani **1,216.24** za nyama ya mbuzi, tani **324.65** za nyama ya kondoo na tani **612** za punda) zilizouzwa katika nchi za Kuwait, Oman, Iraq, Vietnam na Malawi.

**Ndugu Mwenyekiti,** utakubaliana na mimi kwamba ongezeko hili la biashara ya mifugo na nyama halioani na rasilimali ya mifugo tuliyonayo hapa nchini. Hii inatokana na uvunaji mdogo wa mifugo ambao unakadiriwa kuwa pungufu ya asilimia **10** (ng'ombe) kwa mwaka, kiwango ambacho ni chini ya kiwango kinachoshauriwa cha asilimia **15** – **30** kwa mwaka. Hata hivyo, ng'ombe hao huvunwa wakiwa na umri mkubwa (kuanzia miaka 5) na kuzalisha nyama yenye ubora hafifu ukilinganishwa na ubora unaohitajika katika soko maalum. Nafahamu kwamba upo

uwezekano wa kuiongezea thamani mifugo kwa kuinenepesha. Hata hivyo, viwango vya uzalishaji nyama katika machinjio zilizo nyingi na maduka ya kuuzia nyama hapa nchini ni duni. Hii ni moja ya sababu ya nyama yetu kushindwa kuingia soko maalum la ndani na kulazimu kuagiza nyama kutoka nje ya nchi. Mwaka 2015/2016, jumla ya tani **1,492.20** za nyama ambapo tani **836.13** ya ng'ombe, tani **619.46** ya nguruwe, tani **1.0** ya mbuzi na tani **35.61** ya kondoo ziliingizwa nchini. Kinachosikitisha zaidi ni ukweli kwamba sehemu kubwa ya nyama hii inatokana na mifugo inayozalishwa hapa nchini na kuvushwa mipaka kwenda nje ya nchi kwa njia zisizo rasmi, kusindikwa na kurudishwa nchini.

**Ndugu Mwenyekiti,** Sote tunafahamu kwamba sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto nyingi zinazokwamisha juhudi za kuongeza uzalishaji wa mifugo na nyama bora zinazokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje. Baadhi ya changamoto hizo ni upatikanaji wa ardhi ya ufugaji na miundombinu yake, migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, ambayo wakati mwingine husababisha vifo vya watu na mifugo, upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, kuwa na teknolijia za uzalishaji, udhibiti wa magonjwa, ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake, kuwa na muundo imara wa utawala unaowezesha biashara ya mifugo (vyama vya wadau imara), uwezo mdogo wa kimitaji, teknolojia duni, uvunaji mdogo wa mifugo na kwa wakati, uzalishaji mdogo wa nyama inayokidhi viwango vya ubora kulingana na mahitaji ya soko, kutokuwepo kwa mifumo bora ya uzalishaji wa mifugo unaohusisha hifadhi ya malisho bora, uhaba wa viwanda/machinjio za kisasa kwa ajili ya kuchinja, kuchakata na kusindika nyama, utumiaji mdogo wa uwezo wa machinjio za kisasa zilizopo.

Ni dhahiri kwamba uwekezaji katika kutatua changamoto zinazokabili sekta ya mifugo utaleta mabadiliko makubwa na ya haraka. Kwa kuwa bado kuna fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji, hasa pale ambapo mbinu za kibiashara zitatumika kuzalisha mifugo bora kwa kulenga mahitaji ya soko na kuhamasisha uvunaji wa mifugo kwa wakati. Hivyo, ninahimiza wadau wote wanaohusika na maendeleo ya sekta ya mifugo kujikita katika kutatua changamoto zilizopo ili kuongeza kipato cha wafugaji na cha Taifa kwa ujumla.

**Ndugu Mwenyekiti,** nimeambiwa kwamba Kauli mbiu ya mkutano huu ni " **Maendeleo ya Endelevu ya Viwanda** : **Fursa kwa Uwekezaji katika Mnyororo wa Thamani wa Nyama**" hii inamanisha kuwa mna jukumu kubwa la kuhamasisha uzalishaji wa mifugo yenye ubora ambayo endapo itaongezewa thamani basi itatoa fursa za uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vyama na kuongeza pato la Taifa na kipato cha mfugaji. Ninaamini kwamba mtajadiliana kwa kina na kukubaliana namna bora ya kukuweka mikakati ya utekelezaji itakayosimamia vema uendelezaji wa tasnia ya nyama yenye ufanisi na tija kwa taifa. Hivyo, ninasisitiza katika mijadiliano yenu, naomba pia mjikite kujadili namna kuweka mikakati ya kutekeleza katika mambo yafuatayo;

- Kuimarisha vyama vya wadau ili kufikia uwezo wa kuungana na kusimamia uzalishaji wa nyama bora na salama na kuhudumia masoko yenye tija. Kwa kufanya hivi itapunguza chanagmoto ya kukosa mifugo ya kuchinja kwenye machinjio na viwanda vya nyama na kupunguza uingizaji wa nyama;
- Kuhamasisha elimu kwa wafugaji kuhusu ufugaji wa kibiashara na kuvuna kwa wakati ili kupata mifugo bora inayohitajika kuzalisha nyama bora katika machinjio na viwanda vya kusindika na kuongeza thamani ya nyama ili sekta ya mifugo iweze kuchangia pato kubwa kwa Taifa;
- Kuhimiza matumizi ya mizani za kisasa (digital) katika biashara ya nyama ili kuwezesha walaji kununua nyama kulingana na uwezo wake wa kifedha na hivyo kuongeza ulaji wa nyama;
- Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa machinjio za kisasa ,ujenzi wa viwanda vya kusindika nyama na maduka ya nyama yanayokidhi viwango vya ubora . Katika hili naomba Bodi ya Nyama kusimamia ipasavyo kwa kuzifungia bucha na maduka yote ya nyama yasiokidhi viwango vya ubora;
- Kujihusisha kwa karibu katika kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kupunguza au kumaliza kabisa migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na watumiaji wengine kwa kutambua, kutenga, kulinda maeneo ya ufugaji kisheria na kuyaendeleza ili kuhakikisha malisho na maji ya kutosha yanapatikana wakati wote;

- Kuhimiza matumizi ya mashine za kukatia nyama na mizani na kutumia utaratibu wa kuuza mifugo kwa kunadi ili kumwezesha mfugaji kupata bei stahili ya mifugo yake;
- Kuhakikisha biashara isiyo rasmi ya mifugo, nyama na bidhaa zake kwenda nje ya nchi au kuingia nchini kupitia katika mipakani isiyo rasmi bila kufuata taratibu inadhibitiwa;
- Kusajili wadau wote wa tasnia ya nyama ili kazi zao zitambuliwe na mchango wao katika maendeleo ya tasnia ufahamike.

**Ndugu Mwenyekiti,** nawaomba pia wajumbe wa Baraza kushirikiana na watendaji katika sehemu walikotoka kuhusu na utekelezaji wa zoezi zima la utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake kutokana na umuhimu wake katika biashara ya mifugo na mazao yake. Mfumo huu unatumika duniani kote na unahimizwa na Shirika la Kimataifa la Biashara Duniani (WTO) kupitia Shirika la Afya ya Wanyama (OIE) kama mfumo wa kusimamia usalama wa vyakula vitokanavyo na mazao ya kilimo na vyenye asili ya mifugo (SPS).

Aidha, kwa kuzingatia azima ya Serikali ya kukuza uchumi wa viwanda, sekta ya mifugo pia inahamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika nyama na bidhaa zake zenye ubora zitakazoweza kupenya katika masoko maalum (niche market) ya ndani na nje ya nchi. Hivyo, utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo na bidhaa zake ni jambo ambalo haliepukiki na njia rahisi ni upigaji chapa. Kwa sasa Upigaji Chapa ng'ombe ni amri ambayo ni lazima itekelezwe kwa umakini mkubwa kama ilivyoelekezwa na Waziri Mkuu na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ndugu Mwenyekiti,** mwisho kupitia hadhara hii napenda, kutoa wito kwa wadau wote wa Tasnia ya Nyama popote walipo nchini kuhakikisha wanasajiliwa na Bodi ya Nyama Tanzania. Hii itawasaidia kutambulika na kupatiwa huduma mbalimbali na Bodi ikiwa ni pamoja na kuboresha uzalishaji wa nyama na kuunganishwa na vyombo vya fedha pamoja na masoko.

**Ndugu Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza na Wageni waalikwa** Baada ya kusema maneno hayo**,** naomba kuwatakia mkutano mwema wenye ufanisi na mafanikio makubwa na napenda sasa kutamka kuwa Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta ndogo ya Nyama **limefunguliwa rasmi.**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**